

Fomu Ndogo ya Kibali cha Kushiriki katika Utafiti

Unaulizwa kama unataka kujiunga na utafiti huu. Kabla ukubali kujiunga na utafiti, mhudumu mmoja wa timu ya utafiti sharti akueleze mambo fulani kuhusu utafiti huu. Utaelezwa

- a. lengo la utafiti huu
- b. ni nini utakachofanyiwa wakati wa utafiti
- c. muda ambao utafiti huu utachukua na muda ambao utaombwa ushiriki
- d. sehemu zozote za utafiti ambazo ni za jaribio (kitu ambacho kinajaribiwa)
- e. hatari au sehemu zozote za utafiti ambazo zinaweza kukudhuru au kukufanya ujihisi vibaya
- f. faida zozote kwako au kwa wengine ambazo zinaweza kutokana na utafiti huu
- g. matibabu au taratibu zozote ambazo zinaweza kukusaidia badala ya utafiti (njia mbadala)
- h. utambulisho fulani wa mtu ambaye atapewa data yako
- i. kuhusu jinsi usiri na faragha yako ya maelezo yako yatakavyolindwa.

Pia lazima wahudumu wa utafiti wakueleze ikiwa maelezo yaliyo hapa chini yanatumika katika utafiti huu

- a. ikiwa utapokea fidia yoyote (pesa au matibabu bila malipo) iwapo utajeruhiwa ukiwa katika utafiti huu
- b. ikiwa kunaweza kuwa na hatari ambazo hatuzijui kwa sasa lakini zinaweza kutokea baadaye
- c. ikiwa kuna sababu watafiti wanaweza kukuondoa kwenye utafiti huu
- d. gharama zozote kwako kwa kushiriki katika utafiti huu
- e. ni nini hufanyika ikiwa unataka kuondoka kwenye utafiti
- f. wakati utaelezwwa kuhusu matokeo mapya ambayo yanaweza kukusababisha ubadilishe nia yako kuhusu kushiriki katika utafiti
- g. dadi ya watu wataoshiriki katika utafiti.

Baada ya kuelezwa maelezo yote hapa juu, mhudumu wa utafiti atakuuliza kama unataka kushiriki katika utafiti huu. Ikiwa utakubali basi mhudumu wa utafiti atakuuliza utie fomu hii saina. Lazima upewe nakala ya fomu hii iliyotiwa saina kwa lugha yako mwenyewe. Pia utapewa muhtasari ulioandikwa wa utafiti kwa lugha ya Kiingereza.

Wewe au mkalimani wako mnaweza kumpigia _____ kupitia _____ wakati wowote una maswali kuhusu utafiti huu au unachostahili kufanya ikiwa umejeruhiwa. Wewe au mkalimani wako mnaweza kupigia simu kwa Ofisi ya BUMC IRB, nambari ya simu 617-358-5372 ikiwa una maswali kuhusu haki zako kama mshiriki katika utafiti.

Una uhuru wa kuamua kama unataka kushiriki katika utafiti huu au la. Ni kwa hiari yako. Unaweza kuamua kwamba hutaki kushiriki katika utafiti. Unaweza kuamua kutoshiriki katika uchunguzi huu na ujiondoe wakati wowote. Ukiamua kutoshiriki katika utafiti huu au ukiamua kujiondoa hutapoteza manufaa yoyote ambayo unayostahili. Licha ya uamuzi wako hautabadilisha jinsi unavyotendewa na wahudumu lakini ikiwa utaamua kushiriki katika utafiti huu unaweza kubadilisha mpango wako wa matibabu.

Kutia saina hati hii ina maana kwamba ulielezwa kuhusu utafiti huu. Hii ina maana kwamba ulielezwa maelezo yote yaliyo hapa juu. Ukitia saina kwenye fomu hii ina maana kwamba unakubali kuendelea kushiriki katika utafiti huu.

Jina lililochapishwa la mshiriki _____ Saina _____ Tarehe _____

Printed name of witness _____ Signature _____ Date _____